



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



WAKALA WA HUDUMA ZA UNUNUZI SERIKALINI  
(GPSA)

TAARIFA KWA UMMA

WAJIBU WA TAASISI NUNUZI KUJIRIDHISHA NA WAZABUNI WA VIFAA NA  
HUDUMA MTAMBUKA (VHM) KUPITIA MIKATABA MAALUMU.

Dar es Salaam, 27 Februari, 2022.

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) unapenda kuwajulisha Taasisi zote za Umma kuhusu wajibu wao katika utaratibu wa kuwatumia wazabuni wa Vifaa na Huduma Mtambuka (VHM) kupitia Mikataba Maalum baada ya kuwashindanisha bei.

Taasisi Nunuzi wanapaswa kujiridhisha na Mzabuni aliyeshinda kwa kuangalia uwezo wake wa kutekeleza kazi/huduma inayohitajika kama ilivyo kwenye Masharti ya Mkataba kwenye kipengele cha **2(b)** kinachoeleza wajibu wa Taasisi Nunuzi, nanakuu; **"To do due diligence to make sure Suppliers and Service Providers are authorized and capable to perform their duties"**; ikiwezekana hata kumtembelea mzabuni ili kupata maelezo ya ziada yatakayosaidia kujua uwezo wake kulingana na vigezo stahiki kwa wakati huo. Aidha, Taasisi Nunuzi inaruhusiwa kuweka vigezo zaidi kulingana na ukubwa au unyeti wa ununuzi husika kama inavyooleza kwenye Fomu ya Ushindani Mdogo (*Mini-competition Form*) kwenye Kitabu cha zabuni za Vifaa na Huduma Mtambuka.

Ikiwa Mzabuni wa kwanza hatakuwa na uwezo, Taasisi Nunuzi atamtumia anayefuata na kurudia mpaka atakapopata mwenye uwezo.

Wakala unapenda kuwajulisha kuchukua hatua hizi ili kuhakikisha kupata wazabuni wenye uwezo ili kupata Ununuzi unaozingatia thamani halisi ya fedha.

Imetolewa na

AFISA MTENDAJI MKUU  
WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI (GPSA)

Mtaa wa Bohari/Keko Mwanga, S.L.P 9150, Dar es Salaam.

Simu: +255(22)2866071/+255(22)2861617 Barua pepe: ceo@gpsa.go.tz, Tovuti: [www.gpsa.go.tz](http://www.gpsa.go.tz)